HOTUBA YA MKUU WA MKOA WA PWANI, MHE. ABUBAKAR KUNENGE, WAKATI WA UFUNGUZI WA MAFUNZO KWA MAKAMANDA WA JESHI LA POLISI – KIKOSI CHA USALAMA BARABARANI WA WILAYA ZA MIKOA YA PWANI NA DAR ES SALAAM YANAYOFANYIKA MJINI KIBAHA TAREHE 26 SEPTEMBA 2023

Bw. Emmanuel Humba; Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini ya Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi- WCF

Dr. John Mduma; Mkurugenzi Mkuu wa WCF

Kamanda wa Jeshi la Polisi- Kikosi cha Usalama Barabarani Tanzania

Kamanda wa Jeshi la Polisi, Mkoa wa Pwani ; (RPC Pwani)

Makamanda wa Kikosi cha Usalama Barabarani; Kanda (ZTO) na Mkoa (RTO,

Maafisa wa Kikosi cha Usalama Barabarani; Wilaya za Mikoa ya Pwani na Dar es salaam

Watendaji kutoka WCF

Wanahabari mliopo

Mabibi na Mabwana

Nawasalimu kwa jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania!

Formatted: Font: Bold, Not Italic

Formatted: Font: Not Italic

Awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujalia uzima na afya njema na kutuwezesha kukutana katika mji wetu mzuri wa Kibaha kwa ajili ya mafunzo haya muhimu.

Kwa dhati, nikushukuru sana *Mwenyekiti wa Bodi ya WCF pamoja na* Mkurugenzi Mkuu WCF kwa kuamua kufanya mafunzo haya katika mkoa wetu wa Pwani, hususan katika mji wetu wa Kibaha. Pamoja na kuja Kibaha lakini pia mkanialika kuja kufungua mafunzo haya, nawashukuru sana na karibuni sana Pwani, karibuni Kibaha.

Ndugu Washiriki,

Nimeelezwa kwamba mafunzo haya ni ya siku moja na yanalenga kuwapa uelewa kuhusu Sheria ya Fidia kwa Wafanyakazi (Sura ya 263), hususan katika kufahamu mafao ya fidia yanayotolewa na WCF, taratibu za uwasilishaji madai, na umuhimu wa taarifa ya Polisi katika kuchakata madai ya fidia kwa ajali za kikazi zinazotokea barabarani.

Katika hili WCF niwapongeze WCF, kwani mnafanya jambo muhimu sana kwa kuwekeza katika kuwezesha wadau wenu

kuelewa huduma za WCF na taratibu za kuzipata huduma hizo. Ni dhahiri kuwa, wadau wakielewa taratibu zenu wataweza kuzifikia huduma za WCF na kuzipata kwa haraka zaidi.

Ndugu Washiriki,

Hivi leo ninyi mtapata nafasi ya kuelezwa utaratibu mzima wa kuchakata madai ya fidia unaofanywa na WCF na namna ambavyo taarifa toka Jeshi la Polisi zinavyowezesha kuharakisha ama kukwamisha ulipaji wa fidia. Maelezo mtakayopata yataonyesha mchango wenu wa moja kwa moja katika kuhakikisha wananchi au wafanyakazi wanapata huduma ya fidia stahiki na kwa wakati.

Ndugu Washiriki,

Kama walivyosema Viongozi wa WCF, Serikali ilianzisha Mfuko huu (Workers Compensation Fund -WCF) ili kuhakikisha kila mfanyakazi anayepata ajali au ugonjwa unaotokana na kazi anapata fidia stahiki kwa wakati. Napenda kusisitiza kuwa, kuanzishwa kwa Mfuko huu ni takwa la Kikatiba kwa mujibu wa Ibara ya 11 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; ni takwa la Kisera kwa mujibu wa Sera ya Hifadhi ya jamii ya 2003; ni takwa la utekelezaji wa Mikataba ya Kimataifa, hususan Mkataba wa ILO No.102 na No.121.

Ndugu Washiriki,

Kwa namna ya pekee sana, Ilani ya Chama Cha Mapinduzi – CCM (Ibara ya 130), pamoja na mambo mangeni, inaelekeza kuimarisha ufanisi katika hifadhi ya jamii, hususan katika kutoa fidia stahiki kwa wakati. Hivyo, mafunzo haya leo yataonesha jinsi ambavyo taasisi hizi mbili – WCF na Jeshi la Polisi – zinavyochangia Serikali inayoongozwa na Rais wetu mpendwa, Dr. Samia Suluhu Hassan katika kutekeleza Ilani ya Chama Cha Mapinduzi.

Ndugu Washiriki,

Nayasema haya ili muweze kuona ukubwa wa wajibu mlio nao na hivyo muweze kushiriki kikamilifu katika mafunzo ili nia njema ya Serikali ya awamu ya sita, ya kufikisha huduma muhimu kwa wananchi kwa wakati, iweze kutimia kama anayosisitiza Rais wetu mpendwa, Dr. Samia Suluhu Hassan.

Ndugu Washiriki

Naelewa kuwa ili huduma bora ziweze kupatikana ambayo ni haki ya wafanyakazi na wananchi kwa jumla, kuna wajibu wa msingi ambao unatakiwa kufanywa na WCF, Waajiri pamoja na wafanyakazi wenyewe.

Nimetaarifiwa kuwa WCF imeweka utaratibu rafiki sana wa waajiri kujisajili, kuwasilisha michango ya wafanyakazi na kuwasilisha taarifa za ajali ama ugonjwa. Utaratibu huu ni kwa njia ya mtandao ambao hauhitaji mwajiri wala mfanyakazi kupoteza muda wa kutafuta au kufika ofisi za WCF ili kupata huduma. Hivyo, natoa mwito kwa waajiri wote kuhakikisha wanatekeleza wajibu wao wa kujisajili na kuwasilisha michango ya wafanyakazi wao kama inavyohitajika. Vilevile, taarifa za ugonjwa au ajali zifikishwe kwa wakati WCF ili wafanyakazi waweze kuendelea kupata huduma za fidia kwa wakati. Aidha, kwa namna ya pekee sana, natoa mwito kwa wafanyakazi pale wanapopata ajali yeyote barabarani, hata kama ni ndogo, watoe taarifa katika vituo vya Polisi haraka kwani taarifa za Polisi ni mojawapo ya nyaraka za lazima katika kuchakata madai ya ajali zinazotokea barabarani.

Ndugu Washiriki

Kabla sijahitimisha naomba niwatakie ushiriki makini katika mafunzo haya na kuwaomba msisite kutoa maoni yenu yatakayo saidia WCF kuendelea kuboresha ulipaji wa fidia stahiki kwa wakati.

Baada ya kusema hayo, sasa natamka kuwa, mafunzo ya WCF kwa Makamanda wa Trafiki wa Wilaya za mikoa ya Pwani na Dar es Salaam, yamefunguliwa rasmi.

ASANTENI KWA KUNISIKILIZA